

COUNTY GOVERNMENT OF LAMU



THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU

THE HANSARD

Thursday, 18th December, 2025

*The Assembly met at the
Main Chambers, at 2:30 p.m.*

[Deputy Speaker (MCA Paul Kimani Njuguna) in the Chair]

PRAYERS

[Deputy Speaker (MCA Paul Kimani Njuguna): Next Order.

Clerk-at-the-Table: Communication from the Chair.

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

Farewell message to a Member of Staff

[Deputy Speaker (MCA Paul Kimani Njuguna): Honorable Members, I have the following communication to make: -

Honorable Members, the Clerk and Staffs of the County Assembly, it is with a mix of gratitude and deep appreciation that I take this opportunity to bid farewell to one of our esteemed members of staff, Mr Thomas Wanjema who is leaving the service of the County Assembly of Lamu after twelve (12) years of dedicated service. He also served in Lamu County Council for 23 years.

During his tenure, Mr Thomas Wanjema has demonstrated unwavering commitment, professionalism and diligence in the discharge of their duties. His contribution to the work of this Assembly, particularly in the Sergeant at arms (Legislative Department), has been invaluable and has greatly supported the effective functioning of the Institution.

On behalf of the County Assembly, Honorable Members and Staffs I wish to sincerely thank Mr Thomas Wanjema for his selfless service, teamwork and loyalty. His efforts have left a lasting impact and he will be remembered for the positive attitude and dedication to public service.

As he embarks on the next chapter of his life, we extend our best wishes for success, good health and fulfilment in all future endeavors. We trust that the experience gained here will continue to serve as a strong foundation for the journey ahead.

Once again, we express our heartfelt gratitude and wish Mr Thomas Wanjema every success.

MCA Bwana Mohamed Bwana (Majority Leader): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika, ningependa kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza ndugu yetu Thomas Wanjema. Kusema kweli imekuwa siku ngumu sana kwa sababu hizi kuta zote za hili Bunge zinamjuwa Wanjema tangu

ugatuzi uanze na sisi kama Wawakilishi Wadi ama Waheshimiwa kwake tumekuwa kama wanafunzi na pia mlezi wetu. Mimi binafsi kama kiongozi wa walio wengi nimepata mashauri na miongozo mingi sana kutoka kwake na nina Imani hakuna Mheshimiwa hata Mmoja ameweza kukosana naye. Lau kungelikuwa kuna nafasi ya sisi kubaki na yeye hapa Bungeni basi tungeendelea kufanya kazi naye, lakini kama tujuavyo kila kitu kina mwisho. La zaidi ni kumuomba Mungu wakati ambapo anaenda kutangamana na familia yake na tunamtakia kila la kheri na ufanisi katika maisha yake mapya ya uzeeni. Kwa hivyo nina Imani ya kwamba vijana ambao amewaachia hatamu baada ya yeye kuondoka nina Imani kuwa amewaacha na masomo na mafunzo na hata mashauri ya kutosha.

Mwisho ningependa kumhakikisha Wanjema ya kwamba hili Bunge halina kinyongo na yeye kwa hivyo ukiwa na hitaji lolote kutoka kwetu tuko tayari kukusaidia kihali na kimali. Na iwapo kuna yeyote amekosana naye basi kwa niaba ya Bunge ningependa musameheane ili akiondoka hapa awe ameondoka bila ya kinyongo chochote.

MCA Suleiman Mohamed Farah (Witu): Asante sana Bwana Naibu Spika.

Bwana Naibu Spika ningependa kuongezea, kwa hakika hili Bunge limepata pengo kwa sababu nina hakika hakuna Mpambe ambaye ana mwongozo mzuri kama Wanjema na kama yuko basi tutachukua muda mrefu kumzowea. Kwa sababu kibinafsi alikuwa ananipa heshima ya hali ya juu hata kama amenipita kiumri, kwa hivyo nina huzuni mkubwa sana kwa kuona Wanjema anastaafu nikizingatia ya kwamba alikuwa anaheshimu kazi yake kisawasawa.

Vilevile alikuwa mshauri mkubwa sana kwetu sisi Waheshimiwa na nikisema namzungumzia Wanjema basi nitashinda siku nzima kueleza sifa zake. Kwa

hivyo ndugu yangu Wanjema hata kama umestaafu bado tuko pamoja kihali na kimali na ambao wataishikililia nafasi yake basi waige mfano wake. Na iwapo nimekukosea basi naomba msamaha wala usiwe na kinyongo na mimi.

MCA Beatrice Wamaitha Munge (*Nominated*): Thank you Mr Deputy Speaker. Mr Deputy Speaker Sir, you may look at me you can see that am smiling but behind the scene am also crying. I have a mixed feeling because am not going to see a father and a mentor daily and one thing Mr Deputy Speaker and you agree, all of us who are here in this Assembly that Mr Wanjema is a very good time keeper to all of us here in the Chamber. When it comes to work nothing else and it is work and work, in regardless of who you are, political affiliation but he has been a very obedient, loyal and listening to Orders and acting as the order.

On behalf of this Assembly I salute you Mr Wanjema, you have a very good history of Lamu County and I can say that Lamu Assembly will lose a father and a mentor. But I thank God that you are just around the Headquarter, so whenever we need you please it's a matter of a call and be visiting us. Mr Deputy Speaker, I can say that other than his loyalty he has been giving advice to many of us especially on personal matters we appreciate you and we are very grateful.

With those remarks I would say thank you on behalf of this County Assembly that you will be around and whenever you feel that you need to talk to us this door will always be open for you. To the rest of the Sergeants that will be left I know you've mentored them well and am very sure that you are going to take the same footsteps so that they can take Lamu Assembly and Lamu County at large to further steps.

MCA Barisa Deko Bana (Basuba): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kuweza kunipatia fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu wa Baba yetu Thomas Wanjema ambaye aliweza kuhudumu Ofisi za Serikali kwa muda mrefu. Bwana Naibu Spika tunasikitika kuona Wanjema anastaafu na anakwenda kufanya kazi zake za kibinafsi. Kuanzia nichukuwe hatamu ya uongozi 2017 hadi kufikia sasa nimekuwa na mahusiano mazuri na Wanjema na wala hatujawahi kukosana.

Pili ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu Wanjema ameweza kufanya kazi ndani ya Bunge hili letu la Lamu na hakuwahi kupatikana na kashfa yoyote ile. Kwa miaka nilioingia uongozini nilimuona Wanjema kama mtu muadilifu na mwenye hikma na nina Imani wale wenzake anaofanya nao kazi amewapa mafunzo ya kutosha. Kwa hivyo ningewaomba Waheshimiwa wenzangu tuige mfano wa Wanjema ili tutakapomaliza hatima ya uongozi tuwe hatuna kinyongo na yoyote. Mwisho namuomba maisha mema na sisi kama watoto wako tunakuomba utupe radhi na tuweze kuiga mfano mzuri kama wako. Pia ningekuomba Bwana Naibu Spika, Wanjema asitoke Bungeni bila ya kumfanyia sherehe ya kuagana naye kiheshima.

MCA James Njaaga Kariuki (Hindi): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kuweza kunipa nafasi ya kumpongeza ndugu yangu, rafiki yangu na mkaazi wa Wadi yangu ya Hindi. Nina furaha sana kusikia sifa zake kutoka kwa Waheshimiwa wenzangu nikidhania ya kwamba ni mimi peke yangu ndio namjuwa Zaidi lakini kumbe ni kinyume chake. Wanjema analipenda hili Bunge na anaficha aibu zilizoko humu ndani kwa sababu akiwa mtaani anaishi kama raia wa kawaida bila ya kusikiwa akitaja mambo yaliyomo ndani ya Bunge hili. Bwana Wanjema akiwa mtaani anakuwa mstari wa mbele katika kuunganisha wananchi. Jambo ambalo ningekuomba Wanjema ni kwamba ijapokuwa

unastaafu ningeomba ushirikiano wako wa kuendelea kuunganisha wananchi ili tuweze kusonga mbele kimaendeleo. Mwisho nakutakia mazuri wakati utakapokuwa nyumbani kwako na sisi tutazidi kukupenda na namalizia kwa kukusisitiza Bwana Naibu Spika itakuwa vyema iwapo tutaweza kumfanyia sherehe ya kumuaga rasmi Wanjema kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa mwenzangu Barisa Deko Bana. Na iwapo tutakubaliana kumfanyia sherehe basi nitajitolea mbuzi mzima kwa kuwa ni mkaazi wa Wadi yangu na pia kama mfuasi wangu mkubwa.

MCA Mohamed Aboud Abubakar (Faza): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa fursa adhwimu, nikijaribu kuliangalia Bunge hili naona limenyamaza sana hii ni kwa sababu ya kipenzi chetu anataka kutuacha na huu ni huzuni mkubwa sana kwetu sisi Waheshimiwa. Pia Wanjema alikuwa anajuwa kuchunga wakati na kutujali sana hii ni kwa sababu akikukosa Ofisini anakufuata mpaka Ofisini kwako ili aweze kujua chanzo cha kutoingia Bungeni ni nini. Kwa hivyo natumai amewapa mafunzo mazuri wale Wapambe wenzake ili akiondoka waweze kuiga mfano bora kama wake.

MCA Hope Wanjiku Mwaura (Nominated): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika hata mimi nimesimama kumpongeza Wanjema kwa kazi nzuri aliyokuwa akiifanya katika Bunge letu la Lamu. Bwana Naibu Spika, kiongozi wa walio wengi ameweza kutupa historia ya Wanjema na nikiangalia kiukweli amefanya kazi nzuri hapa Bungeni na amekuwa mfano mzuri kwa jamii. Na ninaona amewafunza wafanyikazi wenzake namna ya kuliendesha Bunge kwa ufasaha. Nachukua fursa hii kumuomba msamaha Wanjema najua kuna siku tuliwahi kukwaruzana wakati wa uchaguzi, kwa hivyo nisingependa

astaafu akiwa bado amebeba chuki. Kwa hivyo namtakia kila la kheri na iwapo atahitaji msaada wetu mimi binafsi niko tayari kumsaidia na kinyume chake.

MCA Shekhuna Abbas Shekhuna (Mkomani): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi kama hii ili niweze kumuaga mzee wangu, kipenzi changu Bwana Thomas Wanjema. Nikianza kihistoria Wanjema aliweza kufanya kazi na Babangu mzazi katika Ofisi ya Manispaa miaka ya nyuma kwa hivyo nina haki ya kumuheshimu. Siku ya leo ni siku ya huzuni kwangu kusikia ya kwamba Wanjema anastaafu na lau tungelikuwa na uwezo sisi kama Waheshimiwa ya kumuongezea miaka basi tungemuongezea ili aweze kutuhudumia miaka tuliyobakisha ya uongozi. Lakini tukiangalia hatuna muda kumuacha aende mapumziko tukizingatia miaka aliyonayo haimruhusu kubaki nasi hapa Bungeni. Hata mimi naunga mkono maoni ya Mheshimiwa Deko ya kumfanyia Wanjema sherehe na kumuhudumia kama alivyotuhudumia sisi Waheshimiwa kwa takriban miaka mitatu tuliyofanya kazi naye hapa Bungeni. Namalizia kwa kusema Wanjema hakuwa mkabila ndio maana tunamtambua na kumthamini sana.

MCA Aisha Ali Abdulrahman (Nominated): Asante Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kumpongeza Wanjema kwa sababu amehudumu Ofisi za Serikali kwa miaka mingi sana. Nina masikitiko makubwa sana kuona anatuacha lakini hatuna budi kukubali matokeo kwa sababu muda wake wa kustaafu umefika kulingana na katiba yetu ya Kenya. Mimi binafsi nilikuwa na ukaribu naye kwa sababu nikiingia tu mlango wa Bunge hili ni lazima niende kumtembelea Ofisini kwake na tuweze kuzungumza maneno mawili matatu kabla ya kuingia Ofisini kwangu. Na kama kungekuwa na uwezekano wa kumbakisha Ofisini mpaka sisi tumalize hatamu zetu za uongozi basi tungeweza

kumbakisha Wanjema lakini sharia hairuhusu. Lakini bado tutawasiliana kwa vile bado upo katika Kaunti yetu ya Lamu na uko Wadi ya Hindi kwa hivyo itakuwa wepesi kwangu kukupata. Na Mungu azidi kukufungulia milango ya kheri.

MCA John Mburu Gitonga (Hongwe): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kumuaga Bwana Thomas Wanjema ambaye amekuwa Mpambe tangu Serikali ya Ugatuzi ianzishwe. Na kwa sababu muda wake wa kustaafu umefika basi itakuwa vyema iwapo tutashirikiana sisi Waheshimiwa na kuweza kumfanyia sherehe ya kuagana naye kiustaarabu. Wanjema amekuwa kiungo muhimu kwangu tangu niingie uongozini kwa sababu amenifundisha namna ya kufanya kazi hapa Bungeni na pia anaponikosa Bungeni ananipigia simu ili kujua chanzo cha kutohudhuria kikao cha Bunge.

Ndiposa nikagunduwa ya kwamba anajuwa kusuhubiana na watu vizuri, kwa hivyo ningewaomba wale wafanyikazi wenzake wauige mfano mzuri wa Wanjema. Na kama kutafanywa sherehe ya kumuaga Wanjema hata mimi nitajitolea mbuzi mmoja kama ishara ya upendo kwake. Kwa hivyo namtakia kheri anapokwenda kupumzika na familia yake na kuanza maisha mengine baada ya ajira.

MCA Amina Hassan Bwanamkuu (Nominated): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kumuaga Bwana Wanjema ambaye amekuwa na sisi kwa muda wa miaka mitatu. Mimi binafsi nilipopata habari ya kustaafu kwa Wanjema tangu jana nimeshinda na huzuni kubwa sana. Kwa sababu ameweza kukaa na sisi kama watoto wake na kutupa mafunzo mingi sana ya namna ya kuhudumu kama Mheshimiwa. Na kutokana na ushauri wake nimeweza kufaulu mambo mingi sana katika maisha yangu. Kwa hayo machache ningependa

No. 133

kumuombea maisha mazuri wakati anaenda kustaafu na kujumuika rasmi na familia yake.

MCA Mercy Riziki Nzai (Nominated): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa fursa hii. Kwanza ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuiona siku hii ya leo na tukiwa wazima wa afya. Pili ningependa kumpongeza Babangu Wanjema, kusema kweli kwangu alikuwa kama mzazi na mshauri kwa huu muda mfupi nilioanza kuhudumu kama Kiongozi. Kwa hivyo Bwana Naibu Spika ningependa kumuahidi ya kuwa mashauri yake nimeyazingatia na nitazidi kutekeleza. Pia ningependa kukushauri Bwana Wanjema hata kama umestaafu usibadili mwenendo bali uendelee kuwa na moyo huo huo wa ukarimu na Mungu azidi kukubariki.

MCA Somoe Abdulrahman Mahmoud (Nominated): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii. Kusema kweli sina mengi ya kuzungumza ila nikumtakia maisha mema baada ya kustaafu na Mungu azidi kukulinda na kukuhifadhi.

[Deputy Speaker (MCA Paul Kimani Njuguna): Next Order.

Clerk-at-the-Table: Motion

MOTION

Adjournment

MCA Bwana Mohamed Bwana (Majority Leader): Thank you Mr Deputy Speaker. Mr Deputy Speaker Sir, I beg to move the following motion on the floor of this House:

No. 133

THAT, pursuant to Standing Order 25(3) read together with Standing Order 49(b), this Assembly stands adjourned today Thursday 18th December, 2025 until Monday 2nd February, 2026.

Mr Deputy Speaker Sir, as you are aware that we are in a holiday period and as you understand this holiday includes Christmas and New year events. It will be a great opportunity to us Honorable Members and Staffs to join with their families for the purpose of celebrating these holidays. On my behalf, I would like to take this opportunity to wish all of you Merry Christmas and a happy New Year 2026.

Another thing Mr Deputy Speaker, as we are aware we have extended our calendar because of alot of pending issues like finance bill and supplementary budget. So its high time we adjourn so that us Honorable Members can visit our respective Wards and sit with our electorate and review our development works. Also it is high time for us to engage with our voters in this holiday season.

Secunder

MCA Beatrice Wamaitha Munge (Nominated): Thank you Mr Deputy Speaker and thank you Honorable Members in the House. I stand in support and second this noble motion, it is important that this Honorable House closes and goes for a recess. Mr Deputy Speaker, the only thing that we've not been doing is coming here on daily basis otherwise all other activities will be going on and will have a very good opportunity to have engagement with the Ward Electorates with the citizen of Lamu County. Barely in mind that we are heading to festive seasons, will have ample time to celebrate and spend time with them. On the

same note, during the engagement with the electorates will have a good public participation and therefore it will be for the betterment of our County.

The other issue Mr Deputy Speaker Sir is that, now that we are going for a recess we will not be coming here physically, so some tasks like Committees works will be ongoing and am sure that the responses that we have not received the Clerk will ban the midnight when and make sure that by the time we are coming back after recess in February 2026 all the responses that are pending its my plead with the Assembly that you will receive so that we can give justice to people of Lamu.

Its also a high time that we can be able to do oversight of the Executive, at that time Mr Deputy Speaker will have ample time to visit the ongoing projects so that we can know how Lamu is progressing so that citizens of Lamu can have quality spending of the money and therefore justice should be done because they are paying taxes. We also need to review some policies and research because we have some pending jobs and see what is better for Lamu County. Mr Deputy Speaker Sir, not forgetting that now we are on recess that we are praying your Office that you can do some trainings and capacity building to the Members of Staffs and the Members of this Assembly. So that when we come next year after long recess will be very vibrant, the energy will be more than it was.

Its also a high time that this Assembly can be able to plan for future schedules and sittings. And if the electorates of Lamu are comfortable I can assure you that the electorates of Lamu will also enjoy. With those many remarks I second.

Motion Proposed

Members Contributions

MCA Suleiman Mohamed Farah (Witu): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuunga mkono hoja ambayo imeletwa na Kiongozi wa walio wengi. Kwa hakika tunaamaliza mwaka wa 2025 kwa hivyo ni vizuri iwapo tutakwenda kwa mapumziko ili sisi kama Wawakilishi Wadi tuweze kukaa na wananchi na kusikiliza vilio vyao ili tukirudi Bungeni tuwe tumejipanga kimiradi. Na kama ndugu yangu Beatrice alivyosema hata kama Bunge limefungwa kwa sababu ya likizo shughuli zote zisimame, tunaweza kuja kukalia kamati na shughuli zengine za ndani ya Bunge.

Mover's Response

MCA Bwana Mohamed Bwana (Majority Leader): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika nachukua fursa hii kuwashukuru Viongozi wote ambao wameweza kuchangia mswada nilioleta hapa Bungeni. Na kama tulivyotangulia kuzungumza ni kwamba tumeweza kung'ang'ana na saa hii ni wakati wa mapumziko. Langu kubwa ni kuwaombea ndugu zangu ambao wako hapa Bungeni wawe na Krismasi na mwaka mpya wa kheri tukumbukane kwa maombi. Pia haitakuwa vyema ikiwa Waheshimiwa wenzangu wameweza kujitolea mbuzi kwa ajili ya sherehe ya kumuaga Wanjema na mimi kama Kiongozi wa walio wengi pamoja na Chief Whip tutatowa mbuzi mmoja mmoja kwa ujumla watakuwa mbuzi wanne.

(Question put and agreed upon)

[Deputy Speaker (MCA Paul Kimani Njuguna): Honorable Members, there being no other business, the Assembly stands adjourned until Tuesday 3rd February 2026 at 2:30pm.

The Assembly rose at 5pm